THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# SCHOOL BASED ASSESSMENT

## KISWAHILI SEHEMU B na C

## Gredi ya 7

Septemba 2024

© KNEC 2024

**JINA LA MWANAFUNZI**__________________________________________________

**GREDI** ______________________________________________________________

**TAREHE**____________________________________________________________

**MUDA: SAA 2**

**<u>KWA MATUMIZI YA MTAHINI</u>**

**JEDWALI LA ALAMA**

**SEHEMU B**

| SWALI | ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| UPEO | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| ALAMA | | | | | | | | | | | | |

| | ZOEZI 4: SARUFI | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SWALI | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| UPEO | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 1 |
| ALAMA | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |

| | ZOEZI 5: KUANDIKA |
|---|---|
| SWALI | 28 |
| UPEO | **4 -** Kiwango cha juu cha kutathminia<br>(Performance Level) |
| ALAMA | |

| | SEHEMU C: FASIHI | |
|---|---|---|
| SWALI | ZOEZI 6: FASIHI SIMULIZI | ZOEZI 7: NOVELA |
| UPEO | 10 | 10 |
| ALAMA | | |

**ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **1** hadi la **4**.*

Bila shaka umewahi kupata pesa wakati fulani katika maisha yako. Je, ulizipata vipi pesa hizo? Je, ulipewa na mzazi au mlezi wako kama **masurufu**? Au wewe na wenzako mlikuwa na mradi mdogo, pengine wa kukuza mchicha, kufuga sungura au kuku?

Ni wazi kwamba baadhi ya shughuli tunazofanya katika maisha hutuletea pesa. Pesa hizi hutuwezesha kukidhi mahitaji mbalimbali kama vile kununulia chakula na mavazi. Kadhalika tunaweza kuzitumia pesa hizi kutosheleza mahitaji mengine kama vile kulipia gharama ya matibabu na kuwasaidia walio na mahitaji mbalimbali.

Ikumbukwe kwamba ni muhimu kapangia na kuweka rekodi ya matumizi ya pesa tunazopata. Tukiwa na mpango maalumu wa kutumia pesa, tutajua, kwa mfano, ni lipi la kushughulikiwa kwanza, na lipi la kungojea. Tutajua ni kiasi kipi tutakachotumia na kipi tutaweka akiba. Bila mpango ufaao wa matumzi ya pesa tunaweza kujipata tumelala matajiri tukaamka maskini.

1. Wewe na wenzako mnaweza kupata pesa kutokana na

   ________________________________________

2. Kuwa na mpango wa matumizi ya pesa kuna faida gani?
   A. Mtu anajiongezea maarifa kuhusu miradi ya ufugaji.
   B. Huwafanya wengine watambue yale ambayo tunahitaji.
   C. Huwezesha kujiwekea msingi bora kwa maisha ya baadaye.
   D. Mtu anajifunza kuelewa hali ya jamii yake.

3. Kauli, **tumelala matajiri tukaamka maskini** imetumiwa katika kifungu. Unadhani mtu akilala tajiri na kuamka maskini atafanya nini?

   ________________________________________

4. Eleza maana ya neno, **masurufu**, kuingana na kifungu.

   ________________________________________

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **5** hadi la **8**.*

Hapo zamani wadudu wote waliishi pamoja kwa upendo. Kila mdudu alimthamini mwenzake. Hali kijijini humo ilikuwa shwari.

Usiku mmoja mchwa alisikia mnongono nje ya nyumba yake. Malaika yalimsimama kwa kushtuka. Aliwawazia wanawe waliokuwa wamelala chumbani bila kuwa na mwao na hatari iliyowakodolea macho. Alinyatia hadi chumbani akawapata wako salama. Alirudi sebuleni na kukaribia dirishani kuchungulia.

Lo! Aliona wingu la ndege waliokuwa wamekutanisha vichwa vyao pamoja. Alitega sikio ndi ili kunasa njama yao. Hakuamini alichokisikia. “Ati wanataka kuidhabu jamii ya wadudu.  Wanadai sisi akina mchwa ni waharibifu. Inabidi niwatahadharishe wengine.” Mchwa alijisemea huku akivaa viatu. Alitifua kivumbi hadi kwa jirani yake Nyuki na kushauriana jinsi ya kujiokoa kwa adhabu hii. “Njia ya pekee ya kujisalimisha ni kuhakikisha kwamba tumejenga makao imara. Mimi mzinga wangu utanifaa nawe kichunguu chako ni ngome imara. Wenzetu tutawasaidia kujenga makao ya kudumu. Ila naona ni muhimu tuchunguze na kuepuka mambo ambayo yanaweza kuharibu uhusiano wetu na ndege”. Nyuki alisema.

5. Kulingana na aya ya kwanza, wadudu waliishi katika hali ya:

_______________________________________________

_______________________________________________

6. Ni jambo gani ambalo linaonyesha kwamba mchwa ni mlezi mwema?

_______________________________________________

7. Unadhani wadudu walisababisha uharibifu gani kwa ndege?

_______________________________________________

8. Ni funzo gani unalopata kutokana na **aya ya mwisho?**

_______________________________________________

**UFUPISHO**

*Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la* ***9*** *hadi* ***12****.*

Moja kati ya masuala ambayo yanaathiri jamii ya binadamu ni ulanguzi wa binadamu. Ulanguzi wa binadamu ni hali ya kuwateka nyara binadamu na kuwauza au kuwatumikisha katika kazi za sulubu. Ulanguzi huweza kusababishwa na hali kama vile umaskini. Watu ambao hawana chanzo cha riziki ni mawindo rahisi ya walanguzi wa binadamu. Si ajabu kuwapata watu wakiwachukia hata watoto wa ndugu wa toka nitoke na kuwasafirisha ughaibuni kwa madai ya kuwatafutia kazi.

Ulanguzi wa binadamu una madhara makuu kwa jamii. Tendo hili hupalilia utengano wa kifamilia na dhiki za kisaikolojia. Hali kadhalika, wahasiriwa wa tendo hili hupitishiwa aina mbalimbali za dhuluma kama vile kupigwa na kunyanyaswa kimapenzi.

I**li kukabiliana na ulanguzi wa binadamu ni muhimu kuwa makini ili kuwatambua watu ambao wana nia ya kuendeleza biashara hii haramu. Tuhakikishe tunaishi kwenye mazingira salama.** Aidha **hatuna budi** kupiga ripoti katika vituo vya usalama kuhusu tuhuma yoyote ya visa vya ulanguzi.

9. Kauli ifuatayo imetumiwa katika kifungu: *Ulanguzi wa binadamu ni hali ya kuwateka nyara binadamu na kuwauza au kuwatumikisha katika kazi za sulubu. Ulanguzi huweza kusababishwa na hali kama vile umaskini.*

   Fupisha ujumbe katika kauli hiyo kwa **sentensi moja.**

   ______________________________________________________________

10. Aya ya **pili** inaonyesha madhara ya ulanguzi wa binadamu. Eleza madhara hayo kwa sentensi **isiyozidi maneno 10.**

   ______________________________________________________________

11. Andika ujumbe wa kauli zilizokolezwa rangi katika **aya ya mwisho** kwa sentensi moja.

   ______________________________________________________________

12. Kauli: *'hatuna budi'* imetumiwa katika kifungu. Andika maana ya kauli hiyo kwa **neno moja.**

   ______________________________________________________________

**Geuza ukurasa**

**ZOEZI 4: MATUMIZI LA LUGHA** **(alama 18)**

Usafi ni jambo muhimu 13___ maisha. Binadamu anastahili 14___usafi 15___kuepuka magonjwa 16___ 17___ kuzuia.

13. A. kuhusu B. miongoni mwa C. katika D. mithili ya
14. A. kudumisha B. kudumishia C. kudumishana D. kudumishwa
15. A. kama B. angaa C. lakini D. ili
16. A. ambao B. ambayo C. ambalo D. ambazo
17. A. tutaweza B. tukaweza C. tunaweza D. tukiweza

18. Mnyama nimpendaye ni yule asiyeonyesha ukali. Chagua neno sahihi kujaza nafasi.
Mnyama akitunzwa vyema haonyeshi__________________________(wepesi, ukali)

(alama 1)

19. Jaza nafasi kwa viambishi sahihi. (alama 1)

Nyanja ________mejaa mashabiki wanao___shangilia sisi.

20. Kitenzi kilichopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo ni kitenzi kishirikishi.

Malik alikuwa mchungaji.

Tunga sentensi yenye kitensi kisaidizi. (alama 1)

______________________________________________________________________

21. Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao. (alama 2)

Sewe akifanya utafiti mtandaoni ataandika makala bora zaidi.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

22. Meta amebeba mzigo wa mzee yule.

Kwa hivyo: (alama 1)

A. Meta amebebea mzigo kwa mzee yule.
B. Meta amembebea mzigo mzee yule.
C. Mzigo umebebewa kwa Meta na mzee yule.
D. Mzigo umebebwa na Meta na mzee yule.

23. Jaza nafasi katika jedwali lifuatalo kwa kufuata mfano uliopewa. (alama 1)

| **Sentensi** | **Kukanusha** |
|---|---|
| Wanafunzi wanapalilia maua. | Wanafunzi hawapalilii maua. |
| Taarifa hiyo ilifurahisha | |

24. Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Soma kifungu hiki kwa sauti." Mlezi wangu aliniambia.

25. Unganisha sentensi zifuatazo kuwa sentensi moja. (alama 2)

Maria ametunga hadithi.

Joshua amechora picha.

26. Neno kishamba ni hali ya udogo ya neno shamba. Tunga sentensi ukitumia hali ya ukubwa ya neno: ngoma (alama 1)

27. Kinyume cha neno **ngumu** ni **laini.** Jaza nafasi kwa kinyume cha neno lililopigiwa mstari katika sentensi. (alama 1)

<u>Mgeni</u> aliupokea mkoba wa ________________________

**ZOEZI 5: KUANDIKA** **(alama 10)**

28. Wewe ni katibu Chama cha Watunza Mazingira Chipukizi katika kijiji cha Matendo. Umeshirikiana na chifu kuandaa mkutano kuwahamasisha wanajamii kuhusu matumizi yafaayo ya maliasili. Mwandikie barua rafiki yako kumwalika kwenye hafla hiyo.

## SEHEMU YA C: FASIHI

**ZOEZI 6: FASIHI SIMULIZI** **(alama 10)**

29. *Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali.*

*Lala mtoto ee lalaaa*
*Luluu mwana ee luluu*
*Tazama njianiiii*
*Mama anakujaaa*
*Metoka sokoni*
*Mboga ameuza*

*Mebeba vitamuu*
*Wadhani ni niii?*
*Naona vidizi*
*Vidizi vitamu*
*Viwili ni vyakooo*
*Kimoja ni changu*

*Lala mwana ee lala*
*Usilie mwanaa*
*Wanipa uchunguu*
*Kilio ukitoaa*
*Luluu mwana ee luluu*

a) Wimbo huu ni wa aina gani? (alama 1)

_______________________________________________

b) Eleza sifa **mbili** za wimbo wa aina hii zinazojitokeza katika wimbo huu. (alama 2)

_______________________________________________

c) Eleza shughuli moja ambayo jamii katika wimbo huu inafanya ili kujipatia mapato. (alama 1)

_______________________________________________

d) Eleza sifa **mbili** za mwimbaji wa wimbo huu. (alama 2)

e) Wewe na mwenzako mnawawasilishia wenzenu wimbo huu darasani. (alama 4)

Eleza mbinu **nne** mtakazotumia ili kuufanya uwasilishaji wenu uvutie.

30. **ZOEZI 7: Novela** **(alama 10)**

*Soma kielelezo kifuatacho cha novela kisha ujibu maswali*

Juhudi za Tesi za kutoa huduma kwa jamii zilitambuliwa kote nchini. Video zake akifanya mambo yenye manufaa kwa jamii zilisambaa katika mitandao ya kijamii. Akawa na wafuasi wengi kama mchanga wa bahari.

Umaarufu wa msichana huyo, mwenye umri wa miaka kumi na minne haukuwa wa kuamkia tu. Alikuwa kaulalia. Alikuwa kachanika kwenye mpini kuitumikia jamii yake. Yote yalianzia shuleni, kwa vitendo vidogovidogo tu vya ukarimu; aliwaauni wanafunzi wenzake katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji, kisha kapanda kutoka kidato kimoja cha ukarimu hadi kingine. Hatimaye, Tesi aliwaongoza wenzake kubuni kikundi cha Tufaane. Kikundi hicho kilianzisha mradi wa kupanda mboga chini ya uelekezi wa mwalimu wao. Kikataa chao kilijaa na kusaza aina za mboga zilizonawiri kweli kweli. Si mchicha, si kabeji, si sukumawiki, si munavu hata mchunga na kisamvu zilikuwako.

Kutokana na mboga hizi, Tesi na wenzake waliweza kulisha si jamii ya shule tu bali majirani wa karibu na mbali. Sifa zao zikaenea kote kama moto nyikani. Wenzao wenye mahitaji hawakuachwa nyuma. Kipato kutokana na mauzo ya mboga hizi kilitumiwa kuwanunulia vifaa vya kimsingi vya ujifunzaji. Baadhi ambao walikuwa karibu kuipungia shule mkono wa kwaheri wakaokolewa, nao wakajiona wenye bahati kama ya mtende. Hawakuacha kummiminia Tesi sifa.

**Pamoja na sifa hizi zote, Tesi hakujitanua kifua.** Aliendelea kutia bidii masomoni. Alizidisha matarajio kwa kila tathmini aliyofanya katika Gredi ya 7. Hata alipokuwa amejituliza kwenye kochi moja sebuleni mwao akizitazama video zake, Tesi hakuacha kumshukuru Mungu kwa kumwezesha kutekeleza haya yote. Hakuacha kuuahidi moyo wake kwamba atajifunga kibwebwe kuiboresha hali ya maisha ya jamii yake.

a) Bainisha mandhari ambamo matukio ya sehemu hii ya novela yanatokea.

(alama 2)

b) Suala la uwajibikaji limejitokeza katika sehemu hii ya novela. Toa mfano mmoja kuthibitisha. ( alama 1)

c) Eleza masuala mengine mawili yanayojitokeza katika sehemu hii ya novela.

(alama 3)

d) Kauli**,** *'Pamoja na sifa hizi zote, Tesi hakujitanua kifua'* imetumiwa katika dondoo. Je, kauli hii inadokeza sifa gani ya Tesi? (alama 1)

e) Mwandishi wa kazi ya kifasihi hutumia mbinu mbalimbali kuwasilisha ujumbe. Eleza mbinu **tatu** za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. ( alama 3)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**